



Utangulizi

Kuzaliwa upya ni muhimu sana katika wokovu. Yesu alisema, 'Kweli nakwambia, mtu asipozaliwa upya hataweza kuuona Ufalme wa Mungu' (Yohana 3:3). Kuzaliwa upya kuna maana ya mabadiliko ya moyo na maisha. Ina maana kuwa na imani ya kweli kwa Yesu, ya kwamba ameilipia adhabu ya dhambi. , na kumuamini yeye kuwa ndiye Mwokozi wa kweli; na kwamba ninamtolea maisha yangu kwa Yesu, ninakubali ya kuwa yeye ni Bwana (yeye ndiye anayeyatawala maisha yangu tangu sasa) Sasa kwa hakika nimekuwa mwanafunzi wake, ninakuwa nimeanza kuifuata 'Njia'. Maisha mapya kama muumini wa kweli na mwaminifu na mfuasi wa Yesu sasa yamekwisha kuanza. Neno la kitheologia 'kuzaliwa upya' ndilo linalotumika katika tukio hili. Mtoto hawezi kujitungisha mimba wala mtu yeyote hawezi kujiumba mwenyewe! Roho wa Mungu ndiye afanyaye kazi. Mtu anayetubu mbele za Mungu na kumuamini na kum pokea Yesu kama Bwana na Mwokozi 'anzaliwa na Mungu' (Tazama Yohana 1:13). Hiki ni kipindi cha kugeuka; hakika inaweza kusemwa kwamba hii ni sikukuu ya pili ya mtu kuzaliwa!

Mahusiano Mapya

Mahusiano mapya na Mungu kupitia Yesu Kristo sasa yameanza, na moja ya matokeo yake ni mtazamo mpya juu ya maisha. Mtazamo wa zamani uliharibiwa na kutiwa doa na dhambi, hata kama mtu hapo awali alikuwa katika hali ya, 'kujaribu kuishi maisha mazuri' kwa kutumia nguvu zake mwenyewe. Sasa kuna mabadiliko halisi ya kimaadili, na mara nyingi mabadiliko haya yanaweza kuonekana kwa huyu muumini mpya na kwa watu wengine. Kuzaliwa upya kuna maana ya maisha mapya katika Kristo Yesu – na mchakato huu unaletwa na tendo la neema (zawadi) ya Mungu (tazama Waefeso 2:8-9).

Mtu ambaye hajazaliwa upya ni kipofu kwa habari ya mambo ya Mungu. Kwa kweli 'tatizo' zaidi si kwamba hawezi 'kuona' mambo ya Mungu, ni jambo kubwa zaidi ya hilo. Tunakuwa tumekufa kiroho na hivyo tunapaswa kuzaliwa upya, na hadi pale tunapozaliwa upya, tunabaki tumekufa katika dhambi zetu. Yesu alikuja kuwafanya vipofu waweze kuona (Luka 4:18-21) na hiiina maanaya ziadakatika kuleta maana katika mazingira haya: kukabili upofu wa kiroho na wa kimwili.

Dhambi inakabiliwa kwa njia ya toba na msamaha unaletwa na Yesu pale msalabani; ile asili ya zamani ya uovu inanyang'anywa silaha. (Tazama Zaburi 51:5; Yeremia 17:9; Marko 7:21-23; Yohana 3:3-6; Warumi 6:6 na 8:7-8; 1 Wakorintho 2:14; Waefeso 2:3).

Uamuzi wa kumfuata Yesu, kuwa ni Bwana na Mwokozi (na kumtambua kuwa ni Masihi – Mwokozi aliyetumwa na Baba) ni muhimu na ni tendo la imani. Baada ya toba na imani katika damu ya Yesu, kuzaliwa upya kiroho kunafuata, na ni jambo ambalo ni gumu kwa mwanadamu kuelezea kiufasaha. Mtoto wa Mungu ameweza kuzaliwa upya, '...katika maisha ya matumaini kupitia ufufuo... na urithi usioweza kuharibika, kuteketea wala kufifia (tazama 1 Petro 1:3-4; na pia zingatia ya kwamba kuna mtazamo wa siku zijazo: 'wokovu ambao upo tayari kudhihirishwa' unaotajwa katika mstari wa 5).

Dhana ya kufanywa kuwa 'wana', hapa haijalishi kama mtu ni mwanaume au mwanamke – kwasababu katika kipindi cha bibilia dhana hii iliashiria hali katika maana ya urithi. Hali ya kuwa Mwana (kupokelewa [adoption] kwa neema) inatolewa mara moja tu kwa muumini mpya. Cha kuhuzunisha ni kwamba, wanafunzi wa Yesu ambao wamezaliwa upya wana uwezo wa na pia wanatenda dhambi, na Agano Jipya linatambua jambo hili na linatusaidia kukabiliana na jambo hili. (tazama, kwa mfano 1 Yohana 1:8-9). Bado kuna vita kati ya muumini 'aliyezaliwa upya', na ulimwengu, mwili wa nyama na shetani. Lkini Mkristo aliyezaliwa upya sasa anafahamu ya kwamba kuna vita ya aina mpya, na anafahamu ya kwamba Bwana yupo pamoja naye kwaajili ya kumsaidia kuupinga uovu na kuyashinda mashambulizi ya adui. Baada ya mtu kuwa 'ametereza' au kutenda dhambi yoyote, mwanafunzi wa Yesu anapaswa kuomba msamaha – lakini hii haina maana ya kuzaliwa upya kwa mara ya pili au ya tatu.¹

Tazama Mathayo **18:3**; Yohana **1:12-13**; **3:14-15**; **5:24**; Matendo **3:19**; **4:10**; **16:30-31**; Wagalatia **3:24-26**.

Kama mtoto mwingine yeyote mchanga, mtoto wa Mungu atakua na kukomaa kwa kadiri ya muda unavyokwenda. 'Utakaso' ni jambo linaloendelea katika maisha yote ya muumini. Kunapaswa kuwa na mabadiliko endelevu, kwa kadiri mwanafunzi anapozidi kufanyika kuwa kama Kristo. Je, umekwisha kuchukua ile hatua ya kwanza ya toba na imani kwa Yesu Kristo? Unapokuwa umekwisha kuzaliwa upya, unafahamu kwa undani zaidi ya kwamba, kwa njia ya msalaba na ufufuo wa Yesu, umeokolewa dhidi ya adhabu ya dhambi zako zilizopita. (Tazama maelezo ya chini juu ya 'vipindi vingine' kuhusu Wokovu. Tazama somo Na. 13 juu ya Uhakika. Tazama pia.

2 Wakorintho **5:17**; Waefeso **2:10** na **4:24**; Wagalatia **2:20** na **6:15**; Wakolosai **3:1-10**; 1 Petro **1:22-23**; 2 Petro **1:4**; 1 Yohana **5:11-12**.

¹ Maelezo

Kuna baadhi ya watu ambao wamedai ya kwamba wanafunzi wa Yesu hawawezi kuasi moja kwa moja. Hata hivyo kuna vifungu vingi kwenye Agano Jipya ambavyo vinatoa maelezo tofauti. Zingatia ya kwamba mafundisho ya Yesu juu ya ahera yalitolewa kwenye Injili kwaajili ya waumini. Fikiria juu ya maonyo aliyoyotoa Yesu kuhusu wale ambao hawaja jiandaa kwa ajili ya Ujio wake wa Mara ya Pili. (tazama Mathayo sura 24 na 25). Fikiria matokeo ya Yuda Iskariote. Fikiria juu ya maonyo mengi juu ya uvumilivu. Tazama pia Waebrania 12:25. Muumini anapaswa kuwa ni mtu anayeshinda, si anayetembea katika dhambi na kutokutii. (Tazama Ufunuo 21:7-8). Wakristo wote wanapaswa kwa njia ya maombi kutafuta kuelewa mambo wanayokabiliana nayo hapa duniani kwakuwa hayo ni mambo ya muhimu sana. Kutoka katika Agano Jipya tunajifunza juu ya hali ya kuokolewa kwetu kutoka katika hukumu ya dhambi zilizopita (jambo ambalo lina-tokea pale tunapotubu, kuamini, na kuzaliwa upya), na kuokolewa kutoka katika nguvu ya dhambi (rejea tunzi ya wakati uliopo endelevu; tuna haja ya kuendelea kupigana vita vizuri dhidi ya dhambi, na tuna msaada wa Roho Mtakatifu katika mapigano hayo); na tuna matumaini ya siku zijazo ya kuwa na Yesu katika mahali ambapo hapana uwepo wa dhambi. Kwahiyo 'kuokolewa' hakuna maana iliyo sawa na kuwa 'salama'. Kuanza maisha mapya hakufanani na kuishi maisha hayo kwa uaminifu na kutembea kwa utii. Kitabu kifuatacho kinapendekezwa kuwa ni msaada kwa mafundisho stahili ya bibilia: Once Saved, Always Saved? Na David Pawson. (kimechapishwa na Hodder)Yaani, Je Unapokuwa Umeokolewa, Umeokolewa Moja kwa Moja? Kitabu hiki kinapatikana kwa lugha ya kiingereza.

Copyright © Sovereign World Trust, PO Box 777, TONBRIDGE, Kent, TN11 0ZS, UK
www.sovereignworldtrust.org.uk

Publishing and Translation History

First Published in English by Glory to Glory Publications.

Christian Publications International, PO Box 212, Saffron Walden, CB10 2UU - www.christian-publications-int.com
Editor Peter Sammons. Contributors Alex Jacob, David M. Moore, Peter Byron- Davies, Greg Stevenson, Peter Sammons
ISBN English 978-0-9567831-6-5

This Kiswahili translation for Sovereign World Trust by Revd John Y Madinda with permission
Swahili Edition Published by Sovereign World Trust ISBN - Kiswahili 978-1-908010-12-4